CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI

# SARATANI YA MDOMO WA KIZAZI (CERVIX)



## UTANGULIZI

Saratani ya mdomo wa kizazi ni saratani inayoongoza kwa vifo vingi vya wanawake hapa Tanzania. Pamoja na hali hiyo, saratani hii inatibika iwapo ugunduzi utafanyika mapema.

## NINI CHANZO CHAKE

Husababishwa na aina ya kirusi kinachoitwa Human Papilloma Virus (HPV). Kirusi hiki huambukizwa kwa njia ya kujamiiana na mtu mwenye maambukizi ya Human Papilloma Virus.

## DALILI ZA SARATANI YA MDOMO WA KIZAZI

- Kutokwa na damu baada ya kujamiiana
- Kutokwa na uchafu ukeni
- Kutokwa na majimaji yenye harufu mbaya ukeni
- Kutokwa na usaha ukeni
- Kutokwa na damu isiyo ya hedhi
- Maumivu wakati wa kujamiiana
- Kutokwa na damu ukeni kwa wanawake waliokwisha koma hedhi

## JE, NI TABIA ZIPI HATARISHI ZINAZOWEZA KUPELEKEA MWANAMKE KUPATA UGONJWA HUU WA SARATANI YA MDOMO WA KIZAZI?

- Kuanza ngono mapema katika umri mdogo (chini ya miaka 18)
- Uvutaji wa sigara au tumbaku
- Kuwa na wapenzi wengi, au kujamiiana na mtu mwenye wapenzi wengi
- Kuzaa idadi kubwa ya watoto hasa wanawake walioanza kuzaa wakiwa na umri mdogo (chini ya miaka 18)

## UTAGUNDUAJE MAPEMA KAMA UNA SARATANI YA MDOMO WA KIZAZI

Kwa kufanyiwa uchunguzi wa mdomo wa kizazi kwa wataalamu wa afya angalau mara 1 kwa mwaka.